JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

JARIDA TOLEO NO. 2 | OCTOBA 2023 | HALIUZWI

# TNMC YAWAPIGA MSASA WAUGUZI NA WAKUNGA MKOANI MARA

## Ni Mafunzo ya Sheria na Maadili



# UJENZI WA OFISI ZA TNMC KUKAMILIKA NDANI YA MIEZI KUMI



## Ujenzi rasmi waanza

# HOSPITALI YA RUFAA YA KANDA BUGANDO YANUFAIKA NA MAFUNZO YA UPASUAJI



# BODI YA WAHARIRI


## Mwenyekiti

**Bi.Agnes Mtawa**

## Wahariri

**Happy Masenga,Irene Chilewa**
**Andrew Senge**

## Mratibu

**Andrew Senge**

## Mwandishi

**Mwakapiso Ndimnyaki**

## Msanifu na Picha

**Ezekiel M Nyalusi**


**P.O BOX1736 DODOMA**
**TEL.022-212133975 Fax.022-2133975 Mobile:0786785947**

@tnmchabari www.tnmc.go.tz Info@tnmc.go.tz

# Wauguzi na Wakunga Wapigwa Msasa Juu ya Sheria inayosimamia Taaluma ya Uuguzi na Ukunga na Maadili



Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limetoa mafunzo ya kuwakumbusha wauguzi na wakunga Sheria inayosimamia taaluma na maadili katika mkoa wa MARA na halmashauri zake zote 9. Akizungumza na katika mafunzo ya sheria na Uuguzi Mkoani Mara katika Halmashauri ya wilaya ya Bunda Mji, Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Agnes Mtawa amewataka wauguzi wote Nchini kuzingatia sheria taratibu za uuguzi pindi wawapo katika vituo vyao vya kazi. Sambamba na hilo Bi.Mtawa amewataka wauguzi na wakunga wote Nchini kuhakikisha wanahuisha leseni zao ili kuepukana na usumbufu unaoweza kujitokeza ikiwa ni pamoja na kuondolewa katika orodha ya wauguzi na wakunga Nchini. Kwa upande wake Afisa wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Mwajuma Mutabazi akitoa mafunzo ya maadili amewataka wauguzi na wakunga kuwa na lugha nzuri pindi wanapowahudumia wateja wao ili kuleta ushirikiano bora kati ya mteja na mtoa huduma,pia aliongeza kuwa wauguzi na wakunga ni watu pekee wanaotegemewa katika huduma za afya kwa asilimia 60 hadi 80 hivyo watambue wanalojukumu la kuhakikisha jamii inapata huduma bora na salama. Hata hivyo,Mwanasheria wa Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania Bw.Isaya Nkya akitoa elimu juu ya sheria kwa wauguzi na wakunga amewakumbusha umuhimu wa kulifahamu Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania na sheria zinazo walinda pindi wawapo kazini ili kuwajengea uwezo wa kujiamini pindi wawapo kazini. Naye Afisa Habari wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Ndugu Ezekiel Meshack Nyalusi aliwasihi wauguzi na wakunga kutembelea tovuti ya Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania (www.tnmc.go.tz) pamoja na mitandao ya kijamii ili kuwakikisha wanapata taarifa za msingi zinazowahusu wauguzi na wakunga. Ikumbukwe, Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania limefanya ziara katika mkoa wa MARA ambapo zaidi ya wauguzi na wakunga 400 wamepata mafunzo ya sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010. Huu ni Mkoa wa pili kwa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kutoa mafunzo ya Sheria na maadili katika mwaka huu wa fedha 2023/2024, mwezi Septemba 2023 Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania lilifanya mafunzo kama haya mkoani Tabora katika Halmashauri zake nane(8).Lengo ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na salama,na kuzuia vitendo vya uvunjifu wa Sheria na maadili.baraza linategemea kuendelea kutoa mafunzo haya katika mikoa mingine ya Tanzania bara

# Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania la Saini Mkataba wa Ujenzi na Kampuni ya Strategic Business Solution(Sbs), kwa ajili Ya Ujenzi wa Ofisi za Baraza Dodoma




Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania tarehe 02 Oktoba 2023 limetiliana Saini ya Mkataba na kampuni ya Strategic Business Solution (SBS), kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi litakalojengwa katika eneo la Medeli Makao Jijini Dodoma.Kwa kuanzia kampuni hiyo itajenga jengo dogo lenye ghorofa moja ,litakapo kamilika ,ujenzi wa ofisi kubwa ya ghorofa tano utaendelea Akizungumza wakati wa hafla ya kusaini kandarasi hiyo katika Ofisi za TNMC Jijini Dodoma, Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Bi. Agnes Mtawa, aimeishukuru Menejimenti, Wataalamu wa sekta ya Ununuzi pamoja na sheria kwa miongozo ya kitaalamu iliyofanikisha kukamilika kwa mchakato wa kumpata Mkandarasi. Naye Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Profesa Lilian Msele, ametoa rai kwa mkandarasi kukamilisha ujenzi huo kwa wakati uliokubalika sanjari na kuzingatia viwango na ubora. “Tunatamani jengo likamalike kwa wakati na hata likikamilika kabla ya wakati sisi tutafurahi sana, unajua hapa tulipo tumepanga na tunatumia gharama kubwa hivyo tukikamilisha tutakuwa tume-save fedha nyingi, kwa kweli tumefurahi kwa moyo mmoja na tutakuwa tukitembelea eneo la ujenzi mara kwa mara kuona muendelezo wa kazi” Mkataba huo wa ujenzi unatekelezwa na kampuni yenye hadhi ya daraja la kwanza ya Strategic Business Sulution (SBS) ya Jijini Dar es Salaam ambapo ujenzi huo unatarajiwa kukamilika kwa kipindi cha miezi kumi (10)

# Tnmc yakamilisha Mafunzo kwa Wauguzi na Wakunga wa Chumba cha Upasuaji Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando- Mwanza.





Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limefanya mafunzo ya kuwajengea uwezo wauguzi na wakunga wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando juu ya Utunzaji wa vyumba vya upasuaji na vifaa vyake.Aidha wamejengewa uwezo jinsi ya kutoa usaidizi wakati wa upasuaji Pamoja na kanuni zake.Lengo likiwa ni kuhakikisha vyumba Pamoja na vifaa vinatunzwa vizuri ili kuzuia maambukizi yanayoweza kuleta athari kwa wagonjwa wanaopata huduma ya upasuaji kutokana na changamoto mbalimbali. Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Rufaa ya kanda Bugando mkoani Mwanza Dkt Fabian A.Massaga amehitimisha mafunzo kwa wauguzi wa vyumba vya upasuaji tarehe 06 Oktoba , 2023 ambapo mafunzo haya yamefanyika kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 25.09.2023 yametolewa na wakufunzi kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo Dkt. Massaga amewapongeza wakufunzi kwa kazi nzuri wanazofanya na kuongeza kuwa mafunzo haya yalilenga katika maandalizi wakati wa upasuaji, uandaaji wa vifaa vya upasuaji, uandaaji wa nguo na gozi za kufanyia upasuaji katika chumba cha kutakasia (Central Sterilization Service Department) pamoja na maandalizi ya mgonjwa kabla na baada ya upasuaji (Pre and Post operation preparation) “Mafunzo haya yatakuwa msaada mkubwa kwa Taasisi na pia yataleta mabadiliko makubwa katika chumba cha upasuaji” amesema Dkt.Massaga. Kwa upande wake Bi.Salome Kassanga muuguzi mbobezi katika chumba cha upasuaji na mkufunzi kutoka Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania, amepongeza juhudi kubwa zinazofanywa na Hospitali ya Rufaa ya kanda Bugando katika utoaji wa huduma za afya ikiwemo upasuaji.

Bi.Kassanga ameongeza kwa kusema kuwa Pamoja na mapungufu machache tuliyoyaona, mafunzo haya yataenda kuondoa changamoto nyingi na kushauri mpango wa kufufua vyuo vinavyotoa mafunzo ya huduma za uuguzi katika vyumba vya upasuaji,aliongeza mpango huu wa kuwajengea uwezo wauguzi na Wakunga katika eneo hili utakuwa endelevu na unaweza kuwa suluhisho la changamoto hizi.

# TAARIFA KWA UMMA
# Yah: MAFUNZO YA UTARAJALI 2023/2024
# Dodoma, 09 Oktoba, 2023.

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa lengo la kusimamia Wataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga ili kuulinda umma dhidi ya huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 na Kanuni zake.
Ofisi ya Msajili inapenda kuwataarifu Wauguzi na Wakunga Wahitimu wa mafunzo ya Shahada za kwanza za Uuguzi na Ukunga wanaotarajia kujiunga na Mafunzo ya Utarajali kuanzia tarehe 01.11.2023, kuwa dirisha la maombi kwa njia ya mandao kupitia tovuti ya Baraza (www.tnmc.go.tz) litafunguliwa kuanzia tarehe 16/10/2023 hadi tarehe 20/10/2023.
Wahitimu wenye sifa mnatakiwa kuandaa nyaraka zifuatazo kwa ajili ya kukamilisha maombi na kuchagua Vituo pamoja na kuandaliwa Vyeti ya Usajili wa Awali (Provisional Registration Certificates);

I. Nakala ya Cheti cha kuzaliwa;
II. Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA);
III. Nakala za Vyeti vya elimu ya Sekondari (O-level na A- level);
IV. Nakala za Vyeti vya Taaluma na Leseni hai (kwa waliotoka kazini) na; Passport size yenye ukubwa wa 35×35mm, back ground ya light blue.

Baada ya kukamilisha taratibu za maombi Watarajali wanatakiwa kufika katika Vituo vya Mafunzo walivyopangiwa kuanzia tarehe 01/11/2023 na mwisho wa kupokelewa katika vituo walivyochagua ni tarehe 05/11/2023 ambapo kwa mwaka 2023/24 vituo 31 vinatarajia kupikea watarajali hao.
Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana kwa namba zifuatazo: +255 758 589 706, +255 628 583 890 na +255 787 951 966.

Nawatakia utekelezaii mwema
Imetolewa na:
Happy Masenga
Kny; MSAJILI

# Wauguzi na Wakunga Washiriki katika Kongamano la ECSACONM na HEALCARe




Wauguzi na wakunga kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania,na Nchi Jirani za Afrika mashariki na kutoka bara Ulaya walishiriki Kongamano (Symposium) liliiloandaliwa kwa pamoja kati ya Chuo cha wauguzi na Wakunga Nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini (ECSACONM) na HEALCARe Consortium. Kongamano hilo lilifanyika kwa siku mbili, tarehe 19&20 Mwezi Oktoba 2023 katika Ukumbi wa MABELE. Kauli mbiu ya Kongamano hilo ilikuwa: Do we Treat Our Patients Right? Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Mkutano huo mkurugenzi wa huduma za Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Ziada Sellah ambaye alimuwakilisha Katibu mkuu Wizara ya Afya, amesema kongamano hilo lililoandaliwa na ECSACONM AND HEALCARe Consortium lina lengo la kuhakikisha watumishi wa huduma za afya wanatoa huduma zenye staha zinazojali utu,heshima,upendo na huruma na kujali wateja.Alisistiza kwamba kongamano hili litatusaidia sana sisi wauguzi,wakunga na watoa huduma za afya kuweka huduma dhabiti kati yetu na wateja wetu ili kila mmoja afurahie huduma tunazozitoa" Naye Bi.Agnes Mtawa ambaye ni Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania,na Muwakilishi wa Tanzania katika College ya ECSACONM alieleza kwamba nchi wananchama hukutana kila baada ya miaka minne katika nchi mojawapo ambayo huchaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano.Aidha kila baada ya miaka miwili nchi hizi hukutana kwa kongamano la Kisayansi yaani Scientific Conference ambapo hujadili tafiti mbalimbali ili kuboresha huduma za Uuguzi na Ukunga na namna ya kuboresha huduma.Kongamano la kisayansi litafanyika 2024 Lesotho. Kwa muundo wa ECSACONM kila nchi ina tawi linalotambulika kama chapter,kwa hiyo huu ni mkutano wa chapter ya Tanzania. Bi Agnes aliongeza kwamba"Mara nyingi kupitia mafunzo haya huwa tunajifunza kwa wenzetu jinsi wanavyotoa huduma, nasi tunajifunza kupitia kwao kwasababu katika nchi hizi mifumo ya mafunzo na utoaji huduma tunatofautiana kidogo, lakini pia hata upande wa nyanja ya utafiti

huwa tunabadilishana huku tukitamani huu ukanda tuwe na mambo yanayofanana ili muuguzi au mkunga awe na uwezo wa kufanya kazi nchi yeyote mwanachama ” Kwa upande wake Makamu mwenyekiti wa ECSACONM Bi.Evelyne Maziku amesema “Tunafuraha kushiriki kongamano hili la kisayansi la kitaifa kwa Nchi ya Tanzania huku akiwaomba wauguzi na wakunga wote nchini kuhakikisha anajiunga na mashirikisho hili ili kupata uzoefu ikiwemo kubadilishana ujuzi na mataifa mbalimbali.”

Mwakilishi wa Chapter ya Kenya, Bi.Carren Ombewa ni miongoni wa washiriki walioshiriki katika Kongamano hilo ambapo alifurahia mada zilizotolewa akiwataka wauguzi na wakunga kujiunga na ECSACONM Ikumbukwe ECSACONM inajumuisha Nchi kumi na sita(16) ambazo ni Kenya ,Uganda, Tanzania Zambia Zimbabwe Botswana, Eswatini,Lesotho,South Afrika na South Sudan.Nyingine ni Mauritus,Seychelles,Malawi ,Mozambiq,Rwanda na Namibia.

## Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania lapokea Tanzia ya Wauguzi Watano.

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania anasikitika kupokea taarifa ya VIFO vya Wauguzi na wakunga watano katika kipindi cha mwezi Septemba 2023

1. **Bw.Evarist F. Sanga** (Afisa Muuguzi) Alikuwa akifanya kazi Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila. Alifariki tarehe 27.09.2023
2. **Bi.Solana Ndunguru** -Afisa Muuguzi Msaidizi.Alikuwa akifanya kazi Hospitali ya Mt.Joseph Peramiho.Alifariki tarehe 16.09.2023.
3. **Bw.Robert Benedicto**- Muuguzi,alikuwa akifanya kazi Zahanati ya Kayenze Halmashauri ya Nyang’hwale.Alifariki 11.09.2023.
4. **Magreth Hongoli**-Muuguzi,alikuwa akifanya kazi Hospitali ya Taifa Muhimbili.Alifariki tarehe 05.09.2023
5. **Bi.Leonidas Chano**-Muuguzi,alikuwa akifanya kazi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.Alifariki 03.09.2023.

Wamepigana vita vilivyo vema,mwendo wameumaliza.Mungu azipumzishe roho za marehemu mahala pema peponi.

Bwana alitoa na bwana ametwaa jina lake lihimidiwe.AMEN

## APPLICATION PROCEDURES/STEPS FOR LICENSE RENEWAL

## WHAT TO DO IF I FORGET MY PASSWORD?

**The following are steps for password recovery of the TNMCIS personal account**

1. Step 1: Click on the link "Reset here" found below forgot your password on the login page;

2. Step 2: Enter your email address and click on "Send password reset code", a verification code will be sent to your mobile number (Mobile number that was registered in TNMCIS);

3. Step 3: Enter the verification code in the reset link to confirm your mobile number;

4. Step 4: Now you will be able to reset your password;

5. Step 5: Enter new password. The password field requires a minimum of eight characters, with atleast one uppercase letter, atleast one lowercase letter, atleast one number and atleast one special symbol i.e @, ? , $. %, &, * or #. Example John@124 or Chakechake@360.

**PLEASE NOTE THAT THE VERIFICATION CODE SENT TO YOU IS ONLY VALID FOR 10 MINUTES, SO IF YOU HAVE NOT CLICKED IT WITHIN THIS TIME, YOU WILL NEED TO CLICK ON THE RESET PASSWORD LINK AGAIN.**

# TAARIFA KWA UMMA

## KUSUDIO LA KUWAONDOA KWENYE DAFTARI LA USAJILI NA UOROD-HESHWAJI WAUGUZI NA WAKUNGA AMBAO HAWAJAHUISHA LESENI.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni mamlaka ya kisheria iliyoanzishwa kwa ajili va kusimamia Wataaluma a Taaluma za Uuguzi na Ukunga ili kulinda umma dhidi ya huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga chini.
Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga inayoitwa “The Nursing and Midwifery Act, 2010” na Kanuni zake.
Leseni za Uuguzi na Ukunga zipo kisheria kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 21(1) na (2) na 38(1) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga Na. 1 ya mwaka 2010.
Zoezi la uhuishaji wa Leseni za Uuguzi na Ukunga kwa msimu husika hufunguliwa kila ifikapo tarehe 01 Julai na kukamilika tarehe 31 Disemba.
Baada va kufanva tathimini a zoezi hili imebainika kuwa kuna baadhi ya Wauguzi na Wakunga ambao hawajahuisha Leseni zao.
Ofisi ya Msajili inakusudia kuwasilisha jambo hili katika kikao cha Baraza ili wale wote ambao hawajahuisha leseni zao na hawajatoa taarifa yoyote, ofisi ya Msajili kumjulisha kwamba Wamestaafu, hawatoi huduma za Uuguzi na Ukunga au wamebadilisha taaluma n.k,waweze kutolewa/kufutwa kwenye daftari la Usajili/Uorodheshwaji kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 a Kanuni ya 8(b) ya Usajili, Uorodheshaji na Utoaji Leseni (Registration, Enrollment and Licencing Regulation, 2010).
Aidha, baada ya kuondolewa kwenye rejesta au orodha Muuguzi au Mkunga huvu hatoweza kurejeshwa kwenye daftari la Usajili kabla ya kutimiza miaka mitano (5) kuanzia tarehe aliyoondolewa kwa mujibwa wa Kanuni ya 10(1) na (2) va Usajili,uorodheshwaji na utoaji Leseni (Regisistration,Enrollment and Licencing Regulation, 2010).

Ofisi ya Msajili inawasisitiza Wauguzi na Wakunga wote ambao bado hawajakamilisha zoezi la kuhuisha Leseni kukamilisha taratibu zote ili kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima.
Kwa mawasiliano zaidi tafadhali piga simu na: - +255 787 951 966, +255 682 896 529, +255 628 583 890 na +255 758 589 706.

Nawatakia utekelezaji mwema.

Imetolewa na:
Agnes Mtawa
MSAJILI BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

# CUSTOMER HELP DESK

Have you encountered any challenges regarding our services? Contact us now

## APPLICATION FOR: LICENSURE RENEWAL, PROVISIONAL REGISTRATION, TEMPORARY REGISTRATION AND VERIFICATION

0628583890 , 0758589706 , 0682896529 , 0787204179
0658951966

## APPLICATION FOR: LICENSURE EXAMINATION, INDEXING, AND TRANSCRIPT.

0744377830 , 0753713585 , 0622958841

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**



JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA TOLEO NO 02

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
P.O BOX1736 DODOMA ,TEL.022-212133975
Fax.022-2133975,Email:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA